JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OR-TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI IGOWOLE,
S.L.P 29,
MUFINDI- IRINGA.
TAREHE 28/05/2020.

MOB: +255 755 750 973 Mkuu wa Shule
+255 754 087 454 Makamu Mkuu wa Shule
+255 746 078 389 Mwalimu wa Taaluma
+255 757 091 310 Mhasibu
+255 755 472 893 Matron
KUMB Na. IGSS/AD/VOL. 11/1/24
MWANAFUNZI ……
…….
K.K…….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IGOWOLE HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI MKOA WA IRINGA 2020/2021

Awali ya yote, ninapenda kuchukua fursa hii kukupongeza kwa kufaulu Mtihani wako wa Kidato cha Nne, kitendo ambacho kimekuwezesha kujiunga na Shule ya Sekondari ya Igowole Kidato cha Tano mwaka 2020/2021

Ni matumaini yangu kwamba bahati hii utaitumia vizuri ili uweze kutumia juhudi na maarifa ya hali ya juu kuweza kufanikiwa katika masomo na shughuli nyingine muhimu kama vile uzalishaji mali, michezo n.k

Aidha ni tegemeo langu pia kuwa utakuwa na nidhamu nzuri na utatekeleza na kufuata Sheria, Taratibu na kanuni zote za Shule pamoja na masharti yote ya kujiunga kama yalivyoorodheshwa hapa chini.

MAHALI SHULE ILIPO.
Shule ya Sekondari ya Igowole ipo Wilaya ya Mufindi katika Mkoa wa Iringa. Panafikika kutoka **Dar es Salaam, Morogoro, Njombe, Songea na Mbeya (Tanzania Zambia highway) ukifika Nyololo** teremka. kisha utapata usafiri kwa bei ya Tsh. **3000/= mpaka Igowole Sekondari** ni umbali wa kilometa 17 kutoka Nyololo –**Mufindi**.

Shule ni ya kutwa, ya mchanganyiko wa Wavulana na Wasichana kwa O-level. Ina Hosteli kwa Wanafunzi O-Level na **Bweni kwa Wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita ambao ni Wasichana tu (A-Level).**

HALI YA HEWA NI BARIDI YA WASTANI
Shule itafunguliwa tarehe **…. /…. 2020, Hivyo** Mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni siku hiyo ya kufungua.
a) Alipe karo na michango mingine
b) Arudishe fomu ya ahadi ya mzazi na mwanafunzi
c) Arudishe fomu ya uandikishaji
d) Arudishe fomu za kupimwa, uraia n.k
Ninakutakia maandalizi mema vilevile ninakukaribisha wewe Mwanafunzi na Mzazi /mlezi hapa Shule kwa mashauriano kuhusu ufanisi wa kazi yetu.

……..
INNOCENT GUSTAVOL MGOD.
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI IGOWOLE

KARO YA SHULE
Karo ya shule kwa mwaka ni shilingi **70,000/=** kwa muhula ni Tsh. 35,000/.
Lipa kwenye A/C 6021200063 NMB, BENKI NMB, TAWI MAFINGA
JINA LA A/C IGOWOLE SECONDARY SCHOOL
MICHANGO MINGINE YOTE ILIPWE KWENYE AKAUNTI 60202300398, BENKI NMB, TAWI MAFINGA. PESA TASLIMU HAZITAPOKELEWA.
NB: Fika na BPS (BANK PAYING SLIP) kwa matumizi ya Ofisi ikiwa na Jina kamili la Mwanafunzi na kidato.

MICHANGO MINGINE

1. Fedha za tahadhari shilingi 5000/= ambayo hairudishwi
2. Fedha kwa ajili ya kitambulisho shilingi 6,000/=
3. Mchango wa huduma ya kwanza ni shilingi 10,000/= kwa mwaka kwa mwanafunzi wa bweni
4. Mchango wa ukarabati wa samani 15,000/=
5. Fedha kwa ajili ya Taaluma Tsh. 20,000/=
6. Fedha kwa ajili ya Ulinzi, Wapishi, na vibarua wengine Tsh. 30,000/=
7. Nembo ya shule 2,000/=
8. Mitihani ya mock 20,000/=

Jumla Tshs.108,000.00

Jumla kuu ADA na Michango yote kwa Mwanafunzi wa bweni ni **Tshs. 178,000.00**

MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI NI.

1. Alete ndoo moja kwa ajili ya usafi wa mazingira
2. Cheti cha kumaliza Elimu ya Sekondari (Result slip) Kidato cha nne
3. Kurejesha fomu zilizoainishwa ukurasa wa kwanza
4. Kuleta cheti cha kuzaliwa
5. Flat file moja (1)
6. Bunda mbili za karatasi (Ream DP) A4
7. Kwanja (Slasher)/Panga, fagio aina ya chelewa, fagio ngumu (moppers) na jembe.

SARE ZA SHULE – A-LEVEL

I. Mashati mawili (2) rangi nyeupe tetroni mikono mirefu.
II. Fulana nyeupe ya kuvalia kwa ndani
III. Sketi mbili (2) za rangi maloon (damu ya Mzee iliyokolea) Kitambaa KIZITO. aina ya Linda “Box” mbele na nyuma, pembeni marinda madogomadogo, iwe ndefu ya heshima mpaka chini ya magoti, na koti lake (suti) na Tai rangi ya Maloon.
IV. Jozi mbili(2) za viatu vya ngozi vyeusi visivyo na visigino virefu vya kufunga na kamba.
V. Jozi mbili (2) za soksi nyeupe ndefu “stockings”
VI. Sweta rangi ya Bluu iliyoiva zinapatikana madukani
VII. Nguo ya kazi za nje ni gauni la heshima lisilobana na livuke mpaka chini ya magoti kitambaa rangi ya DARK BLUE. Shamba dress
VIII. Kwa msichana wa kiislamu Hijabu nyeupe nusu kanzu tetroni isiyoangaza suruali pana rangi ya maloon / sketi ndefu maloon
IX. T-shirt zenye nembo ya Shule zinapatikana hapa Shuleni kwa gharama Tshs 10,000/=
X. Nguo za michezo raba, bukta, sketi.
XI. Tracksuit rangi nyeusi YENYE MISTARI MIEUPE ni lazima iwe pana tafadhali.
XII. Jacketi la dukani rangi ya Bluu au jeusi Lisilokuwa na maandishi yoyote.
XIII. Begi la kubebea madaftari “School Bag” rangi Nyeusi.
NB: Vitu vyote vitakaguliwa afikapo.

HAIRUHUSIWI:

i) Vazi lingine lolote nje ya sare za Shule likivaliwa Shuleni hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.
ii) Hereni, mikufu, Pete, shanga, bangili, n.k. Haviruhusiwi kuvaliwa shuleni.
iii) Hairusiwi kuwa na nywele ndefu.
iv) Hairuhusiwi kuja na simu Shuleni Endapo ukikamatwa simu itavunjwa na utapewa adhabu sitahiki.
v) Hairuhusiwi kupaka rangi kucha, wanja machoni au kujichubua kwa mkorogo (“Black is beauty)

MAHITAJI YA MWANAFUNZI WA BWENI KWA MATUMIZI BINAFSI.

1: Godoro moja (1) la futi 2 ½ kwa futi 6
2: Blanketi zito kwa ajili ya majira ya baridi
3: Shuka mbili za kulalia rangi ya bluu na moja ya rangi nyeupe “Bed cover”
4: Mto na foronya rangi ya bluu na chandarua.
5: Taulo, Mswaki, Sabuni, mafuta n.k
6: Sahani yenye kifuniko, bakuli, kikombe, kijiko na thermos
7: Ndoo na beseni kwa matumizi binafsi
8: Tranka (Sanduku la chuma/ bati) kuwekea vifaa vyake

9: Shule inatumia umeme wa Grid unashauriwa mwanao kuja na Taa ya solar au taa inayotumia betri endapo umeme ukikatika kwa ajili ya kujisomea usiku.

10: Madaftari counter books idadi 10 na Mathematical set na scientific calculator.
11: Fedha zake za matumizi binafsi
12: Vitabu vinavyomfaa kununua inapobidi rejea ukurasa wa mwisho.
13. Pasi ya Mkaa kwa ajili ya kunyoshea nguo.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE KWA WANAFUNZI WOTE

A: MAHUDHURIO

Kuthamini muda wa kuwepo mahali unapotakiwa kwa mujibu wa ratiba au maelekezo kutoka uongozi wa Shule.
i) Kuwahi kufika shuleni na kuwepo mstarini kwa muda uliopangwa
ii) Kuhudhuria Shuleni kwa muda wote wa masomo
iii) Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa
iv) Kuhudhuria kazi zote za mikono na michezo
v) Kuhudhuria mikutano ya shule (mfano baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, maandamano, vikao vya madarasa na vikundi mbalimbali vinavyo tambulika kisheria (mfano vilabu vya masomo (Subject clubs), dini n.k)
vi) Kuitika miito ya dharura mara moja

B. HESHIMA

(i) Kuwathamini na kuwaheshimu wanajumuiya wote bila kuangalia umri wao
(ii) Kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita au kuingia mahali ulipo
(iii) Kutumia lugha nzuri wakati wote
(iv) Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wengine katika kazi
(v) Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote
(vi) Kuitika na kukimbilia aliko mkuu aliyekuita
(vii) Kuheshimu Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa vyama na Nembo ya Taifa
(viii) Kuheshimu taratibu za Mikutano, Ofisi za Shule, mali ya binafsi na mali ya umma
(ix) Kukaa kimya darasani na kutoka nje kwa ruhusa ya Mwalimu au Kiongozi aliyekuwepo darasani
(x) Kusimama kwenye mstari wakati wakupokea huduma
(xi) Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo ndani au nje ya Shule
(xii) Baadhi ya tabia ambazo haziruhusiwi kwa Mwanafunzi ni kama zifuatazo: -

a) Kuvuta sigara, kutumia madawa ya kulevya, pombe n.k
b) Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu, kupaka rangi kucha, wanja, kujichubua
c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima au yasiyokubalika
d) Kugombana, kutukukanana, kupigana n.k
e) Uasherati, wizi, utapeli n.k
f) Nguo fupi au nguo ya kubana yenye kuonesha maumbile ni marufuku hapa shuleni

C. SARE

Unapaswa kuwa na sare za Shule kwa mshono unaokubalika na kwa wakati kama utakavyopangiwa kwa;
(i) Wakati wa masomo darasani
(ii) Safari zote za nje kwa jina la Shule
(iii) Wakati wa kwenda Hospitali
(iv) Wakati wa mashindano
(v) Unatakiwa kuwa na nguo za michezo na vazi la kazi za mikono, gauni la Dark Blue kama utakavyo elekezwa

D. MIPAKA YA SHULE

(i) Unapaswa kufahamu mipaka ya Shule na kutokutoka nje ya mipaka hiyo bila kibali maalumu, baada ya kufika shuleni
(ii) Kibali cha ruhusa kitatolewa na mwalimu wa zamu au walimu wa malezi
(iii) Wanafunzi wasitembelee ofisi ya walimu, maabara, nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu bila kibali cha wahusika.
(iv) Hairuhusiwi kabisa kwa mwanafunzi kutembelea

a) Vilabu vya pombe
b) Majumba ya starehe
c) Majumba ya kufikia wageni

E. MAKOSA YANAYO WEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI

a) Wizi
b) Uvutaji bangi na madawa ya kulevya
c) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
d) Kuwekwa unyumba au kuolewa
e) Utoro wa Shule wa muda mrefu
f) Uasherati/ Ugoni
g) Makosa ya jinai
h) Kupata mimba au Kutoa mimba
i) Ulevi wa aina yoyote
j) Kupigana au kupiga au kugombana au kutukanana
k) Kudharau Bendera ya Taifa
l) Kufanya jaribio lolote la kujiua
m) Utovu sugu wa nidhamu kwa ujumla
n) Kufanya makosa ya kujirudia rudia
o) Kugoma au kuchochea au kushawishi mgomo wa aina yoyote kwa Wanafunzi au Wanajamii wanaomzunguka
p) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya Shule.
q) Kushiriki Matendo ya Uharifu, Siasa, Na Matendo yote yanayovunja Sheria za Nchi.
R) Kutembelea majumba ya Starehe, na Nyumba za kulala wageni.

F. UGONJWA

Wagonjwa wote watapata kibali cha kwenda Hospitali kupitia Ofisi ya malezi au Tabibu wa Afya (Clinical officer)
Endapo ana KADI ya BIMA ya Afya ni vyema akaja nayo na wale wasiokuwa nayo wanahimizwa kuunda vikundi vya wanafunzi **SITA** kila mwanafunzi atachanga shilingi **5000/=** ili waweze kulipia na kupewa kadi ya Bima ambayo itarahisisha gharama za Matibabu wawapo Shuleni.
Endapo mwanafunzi atalazwa mzazi atafahamishwa kwa taratibu zingine.

G. USAFI

Usafi ni jukumu la kila mwanafunzi kama sehemu ya maisha yake ya kila siku,hivyo utashughulikia;
a) Usafi binafsi wa mwili na mavazi yako
b) Usafi wa maeneo yafuatayo kama utakavyopangiwa; ukumbi wa chakula, mabweni, vyoo, madarasa,maabara, viwanja na barabara.
c) Vyakula viliwe ndani ya bwalo la chakula tu.

H. MAANDALIZI YA KUBORESHA TAALUMA

Kila mwanafunzi ajiandae kitaaluma (sambamba na combination ya masomo) na kuwa na mahitaji muhimu ya darasani kama**; Daftari (counter books 10), kalamu, Scientific calculator mathematical set**, na ni vizuri pia kama utaweza kupata vitabu vya kukusaidia katika masomo yako.**Vitabu muhimu kwa kila somo vimeorodheshwa na kuambatanishwa na maelezo haya.**

MENGINEYO:

1.Ikipita **tarehe …/…/2020** kama haujaripoti Shuleni utakuwa umepoteza nafasi yako.
2.Mzazi wa mwanafunzi anayo haki ya kufuatilia **mahudhurio, maendeleo, tabia na mwenendo wa mwanafunzi Shuleni** kwa kuwasiliana na Ofisi ya Mkuu wa Shule.
3.Wageni wa wanafunzi wakati wapo Shuleni lazima waonane kwanza naMwalimu wa zamu/wa Darasa/Bweni au Matroni ambaye amepewa uwezo wa kukubali au kutokubali kuonanana Mwanafunzi.
4.Huruhusiwi kuja na vitu vifuatavyo shuleni;
a) Simu ya mkononi
b) Pasi ya umeme
c) Masanduku makubwa (hakuna nafasi bwenini)
d) Nguo zisizo za shule
e) Ukija navyo utarudisha nyumbani kwa gharama zako mwenyewe au vitachukuliwa.
Ninakutakia maandalizi mema na kuwakaribisha wote mzazi na mwanafunzi katika jumuiya ya shule.

MATUMIZI YA UTUNZAJI WA MALI YA SHULE NA MAZINGIRA

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kutumia na kutunza mali ya Shule kama vile; majengo, viti, meza, madawati, majembe, ndoo, vitabu,vifaa vya maabara, n.k

b) Hakikisha kwamba taa za umeme zimezimwa wakati wote mchana.
c) Kisima cha maji kifunikwe baada ya matumizi
d) Weka mazingira ya Shule kuwa safi na ya kuvutia. Okota karatasi na uchafu wote. Pita kwenye njia za miguu, Usikatishe katishe ovyo na kukanyaga maua au majani yaliyooteshwa.

UTORO

Mwanafunzi ambaye hatahudhuria Shuleni bila taarifa atahesabiwa kuwa ni mtoro. Taarifa kuhusu mwanafunzi asiyehudhuria Shuleni kutokana na matatizo yoyote lazima ziwasilishwe Shuleni siku hiyo ya matatizo kwa Mwalimu wa zamu au Walimu wa malezi na Mzazi/Mlezi anayetambuliwa na Shule kulingana na fomu za usajili.

MASHARITI YA KUJIUNGA NA BWENI

Pamoja na sheria na kanuni muhimu za shule unapaswa;

1. Kukubaliana na sheria na kanuni zote za shule
2. Kufuata ratiba ya siku kwa mwanafunzi wa bweni
3. Kuhudhuria **"Roll-calls"** zote kama inavyopangwa na walezi
4. Kuhudhuria **"Preps"** na vipindi vyote vya darasani
5. Kuishi kwa amani, upendo na ushirikiano wa kidugu na wanajumuiya wote
6. Kula **"Menu"** moja iliyoandaliwa na Shule bila kuleta usumbufu wa kujichagulia chakula.

CHAKULA KIKUU HAPA NI UGALI NA MAHARAGWE.

7. Kuchangia gharama za matengenezo ya uharibifu wowote inapolazimu.
8. Kutomleta au kumwingiza mgeni yeyote ndani ya bweni (wanafunzi wa kutwa ni miongoni mwao)
9. Kutoleta au kukaa ndani ya bweni bila ruhusa ya walezi wakati wa masomo
10. Huruhusiwi kupika chochote
11. Ni marufuku kwa wanafunzi wavulana kuingia bweni la wasichana
12. Kutokulala nje ya Shule bila kibali cha **Mkuu wa shule**
13. Kutoka nje ya shule bila kibali maalumu cha **utawala**
14. Kuvaa sare ya shule wakati wote wa vipindi na awapo nje ya mipaka ya shule. (kwa shughuli binafsi, shule au kidini)
15. Kuvaa sare ya nje (shamba dress) baada ya saa za masomo ndani ya mipaka ya shule.
(Shona gauni la heshima rangi ya dark blue lisilobana, lazima livuke magoti na si vinginevyo)
16. Zingatia **UHURU WA KUABUDU "Kumcha MUNGU ni chanzo cha maarifa, hekima, busara, utu wema, uadilifu, upendo, amani na uaminifu**. Unaruhusiwa kuabudu kwa kadri ya dini yako ila usivunje sheria na taratibu zilizowekwa hapa shuleni.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI IGOWOLE
FOMU YA KUKUBALI (FOMU HII IRUDISHE SHULENI)

1.Mimi……kidatocha……..…nimekubali kujiunga na shule ya sekondari Igowole nikiwa mwanafunzi wa bweni.
2. Ninakubali masharti yote, nina ahidi kufuata sheria zote za shule.
3. Niko tayari uongozi wa shule kuchukua hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunirudisha kwa mzazi/mlezi endapo nitakiuka masharti yaliyomo.
4.Sahihi ya mwanafunzi……. tarehe……...

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

1. Mimi……...nina kubali mtoto wangu……. wa kidato cha ……...mwaka……kujiunga na sekondari ya Igowole kuanzia tarehe ……...akiwa mwanafunzi wa bweni.
2. Ninakubali masharti yaliyomo katika kujiunga na bweni ikiwa ni pamoja na kulipa karo yote ya shule na kumtimizia mahitaji mengine ya shule.
3. Nitakuwa tayari kumpokea mtoto wangu wakati wowote endapo atakiuka masharti yaliyomo au kubainika kuwa na afya isiyoridhisha ambayo itahitaji ukaribu wa matunzo ya mzazi /mlezi mwenyewe.
4. a) Anuani yangu ya kudumu ni
……
……
…….....
b) Jina na anuani ya mlezi wa karibu mjini Iringa ambaye shule inaweza kuwasiliana naye katika matatizo mbalimbali ya mtoto
ni……
……
……
……
……
5. Sahihi ya mzazi /mlezi……tarehe……

IGOWOLE SHULE YA SEKONDARI
FOMU YA KUPOKELEWA SHULENI

1. Jina kamili……

2. Mahali ulipozaliwa……...

3. Tarehe ya kuzaliwa……

4. Uraia……

5. Anuani ya nyumbani……...…….

6. Jina la mzazi /mlezi……...

7. Anuani ya mzazi/mlezi (kama tofauti na hiyo hapo juu) ……

8. Ndugu wa karibu. Anuani yake, kitongoji/mtaa……...

Jina	Uhusiano	Anuaniyake	Simu
1…….....	…….....	……	…….....
2.....	.....	.....	.....
3.....	.....	.....	.....
4.....	.....	.....	.....

9. Dini .....

10. Kidato alichopokelewa.....

11.Shule uliyotoka…….....

12.Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama mpira wa miguu, mpira wa mikono, riadha, kuimba, n.k.....

13. Wilaya unakotoka…….....mtaa……...kata…….....

14.Sahihi ya mwanafunzi……tarehe……

15.Sahihi yamzazi/mlezi……tarehe……

Matumizi ya ofisi

Namba ya shule……

Namba ya mtihani……...

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION
IGOWOLE SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 29 MUFINDI-IRINGA

To be completed by medical officer.

Full name……
Age……Years……Sex……
Blood count (Red and White) …….....
Stool examination…….....
Urine analysis……
Syphilis test……
Eye test……
T.B test…….....
Ears……
Chest……
Spleen……
Abdomen……....
ADDITIONAL INFORMATION eg physical or chronically family
disease, etc……
……
……
I certify that the above named student is fit to peruse studies
Signature……
Designation……
Section…….
Date……
NOTE: Medical officer at the time of examination the individual for any aliments you note.
PUPILS:
You must bring this complete form when you come to school, no pupil may enroll without certificate of physical fitness.

……
HEADMASTER IGOWOLE
SECONDARY SCHOOL

IGOWOLE SECONDARY SCHOOL
ESSENTIAL REFERENCE BOOKS/TEXT BOOKS FOR A-LEVEL STUDENTS.

A.HISTORY

1. Major issues in Africa History-ICD
2. Major Events in Africa History-Mwaijage
3. The Political Economy, Imperialism-by Nabudere
4. Africa since 1800-4th edition-by Roland Oliver and Atmore
5. The making of modern Africa Vol .1
6. How Europe underdeveloped Africa- W.Rodney
7. The 20th century –by Duff.M.N
8. Europe from 1815 –by Peacock

B.GEOGRAPHY

1. Certificate Geography (Oxford) Form 3-by Mary Mugo , Robert Karuggah and Paul Kibuuka.
2. General Geography in diagrams –by R.B.Bunnet
3. Regional Geography-by Nyambali/Nyangwine
4. Photography Interpretation and Elementary Surveying for Secondary Level New Edition-by S.E.Dura
5. Certificate Human and Economics Geography-by Morgan and Leong Chang

C.KISWAHILI

USHAIRI

1. Kimbunga-G.Gora (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili –TUKI) 1994
2. Chungu Tamu-T.A.Mvungi. (Tanzania Publisher House) 1985
3. Mapenzi Bora-S.Robert (Mkuki na Nyota) 2003
4. Fungate ya Uhuru-M.S. Khatibu (Macmillan and Aidan)

RIWAYA

1. Vuta n'Kuvute-Shafi .A.Shafi (Mkuki na Nyota)1999
2. Kufikirika –S.Robert (Mkukin a Nyota) 2003
3. Mfadhili –Hussein Tuwa (Mathew B/W and Stationery) 2007
4. Usiku utakapokwisha- Mbunda Msokile (Macmillan and Aidan) 2007

TAMTHILIYA

1. Morani-E.Mbogo (DUP)
2. Kivuli kinaishi-Said Mohamed (Oxford University Press)2007
3. Kwenye Ukingo wa Thim-E.Hussein (University Press)
4. Nguzoya Mama-DUP (1982)

D. GENERAL STUDIES

1. General Studies (Communication Skills for A-Level –M. Kadeghe)
2. General Studies notes (for A-Level Fir V & VI) G. Mshiu and N. Nyagwine

E. ENGLISH LANGUAGE

1. A Complete course for Form V & VI –Michael Kadeghe
2. English for Form V &VI – by Michael Kadeghe
3. Teaching English as a Foreign Language – G. Broughton et. Al
4. A grammar of Contemporary English – Quirk, et. Al
5. Longman English Grammar- L. G Alexander
6. The real English textbook for Advanced Level- by M. Kadeghe
7. Advance English Dictionary

PART II

A. NOVEL

1. The Beautiful One Are Not Yet Born- A. K Amah
2. A Man of the People – C. Achebe
3. Divine providence- Mkuki na Nyota

4. Encounters from Africa – Macmillan
5. The Rape of the Peal- Macmillan

B. PLAYS/ DRAMA

1. An Enemy of the People – H. Ibsen
2. I will marry when I want- EAEP
3. Rwanda Magere- by Okot Omtatah (1991)- Heinemann,Kenya
4. The Bride – EAEP
5. Black Mamba – EAEP

C. POETRY

1. Selected Poem from institute of Education
2. The Wonderful Surgeon and other Poem – Mkuki na Nyota

F. ADVANCED MATHEMATICS.

1. CHANDI I & II
2. BACKHOUSE I & II
3. PURE MATHEMATICS I & II
4. UNDERSTANDING ADVANCED MATHEMATICS

G. ECONOMICS

1. AMBILIKILE – NEW SYLLABAS -2009
2. MORDEN ECONOMIC –ROBERT MUDIDA
3. ECONOMIC 1 ACTIVE - ZISTI KAMILI 2010 SYLLABUS
4. ECONOMIC 1I ACTIVE - ZISTI KAMILI 2010 SYLLABUS
5. ECONOMIC A/LEVEL PAPER 1 AND PROFESSIONAL STUDIES – C.M. AMBIKILE NEW SYLABUS
6. ECONOMIC A/LEVEL PAPER 1I AND PROFESSIONAL STUDIES – C.M. AMBIKILE NEW SYLABUS